## Maswali

1. Waajiri walienda wapi kutafuta wafanyi kazi?
2. Kawaida malipo ya kazi ya siku moja ilikuwa nini?
3. Mbona mwenye shamba alienda sokoni asubuhi?
4. Walisikizana nini na watu?
5. Mwenye shamba alienda kwa soko tena?
6. Ilipofika jioni watu gani walipata mshahara kwanza?
7. Wafanyi kazi walilipwa mshahara sawa, ngapi?
8. Mbona walioajiriwa kwanza walilalamika?
9. Hili fumbo lina maana gani?

## Majibu

1. Kwa soko ya nyumbani.
2. Kwa siku moja malipo yalikuwa senti moja.
3. Kuajiri watu wamfanyie kazi shambani.
4. Kwamba watafanya kazi kwa senti moja kwa siku.
5. Ndiyo, alienda mara nyingi akichukuwa watu waliokuwa wakizembea sokoni.
6. Walioajiriwa mwisho.
7. Watu wote walilipwa sawa, senti moja.
8. Walilalamika kwa sababu walifikiria kwamba watalipwa nyingi kwa kufanya kazi kwa mda mrefu.
9. Mungu atalipa watu sawa – Uzima wa milele. Haitajalisha kama wamekuwa mitume kwa miaka mingi au siku chache.

**SHULE YA JUMAPILI YA CBM**

**Awamu ya 1 Mwaka wa 2**

# 40 Wakulima shambani

## Marejeo

Mathayo 20:1—16

## Kiini cha somo


Kuonyesha kwamba Mungu huwapa zawadi wanaofuata Yesu kwa upendo sio kwa kufanya kazi tu.

## Maneno maalum

1. Muajiri + mahali pa soko + wanaume + kazi + senti
2. Mwenye shamba + senti + wanaume wengine + kazi
3. Machweo + wazembe siku mzima + fanya kazi shambani
4. Kubali + wanaume + senti
5. Jioni + lipa wakulima + mwisho kwanza-kwanza mwisho + wote senti moja
6. Wakulima walioajiriwa kwanza walalamika + malipo sawa kwa wote.
7. Mwenye shamba + lipa anavyopenda + tumikia Mungu.

**40.1** Wakati wa Yesu kazi nyingi zilkuwa za kibarua. Waajiri walienda sokoni kutafuta waliotaka kazi. Malipo yalikuwa kwa senti. Hii ilkuwa malipo ya kazi ya shamba kwa siku moja. Ililipwa mwisho wa kila siku.

**40.2** Yesu aliwambia hadithi ya mwenye shamba alieenda asubuhi moja kutafuta watu wa kuajiri ili wamfanyie kazi shambani. Alikubaliana nao kulipwa senti moja baada ya kazi ya siku. Akawapeleka shambani. Baadaye alirudi sokoni na akapata watu walikuwa wamesimama na kuzembea tu hawana kazi. Hata nao aliwaajiri na akawapeleka shambani wafanye kazi. Alirudi soko saa sita tena saa tisa mpaka jioni akiwauliza kama nao walitaka kazi,na kila wakati aliwambia, “Hata nyinyi enda kwa shamba langu mfanye kazi na nitamlipa malipo ya kawaida.”



**40.3** Kabla ya machweo alirudi sokoni tena akapata watu waliokuwa wamesimama kule, “Mbona mmezembea siku mzima bila kazi.” Walimjibu, “Kwa sababu hakuna mtu ametuaajiri.” Mwenye shamba aliwaambia, “Nyinyi pia enda mfanye kazi kwa shamba langu.” Kwa hivyo walienda.

**40.4** Kila wakati huyo mwenye shamba aliwaajiri watu kufanya kazi aliwambia kwamba atawalipa bei ya kawaida ya siku –senti moja.

**40.5** Ilipofika jioni saa ya kulipa watu waliomfanyia kazi mshahara, alianza na wale waliokuja mwisho. Walikuwa wamefanya kazi kwa saa moja tu. Mwenye shamba aliwalipa senti moja kila mtu. Halafu akawaita wale waliokuja alasiri. Walikuwa wamefanya kazi kwa saa chache saidi. Nao walilipwa senti moja kila mmoja. Baadaye aliwaita walioajiriwa kwanza. Walifikiri watalipwa zaidi kwa sababu walikuwa wamefanya kazi kwa siku mzima. Walikuwa wamefanya kazi kwa jua kali mchana wote. Lakini mwenye shamba aliwapa senti moja tu kama wengine. Wote waliofanya kazi kwa siku hiyo walipata mshahara sawa, wa senti moja.

**40.6** Waliofanya siku mzima walilalamikia mwenye shamba. Walisema, “Umetupa malipo sawa na hali sisi tumefanya kazi kwa masaa mengi.” Mwenye shamba aliwajibu kwamba walikuwa wameelewana malipo ya senti moja. Tena akasema, “Ninaweza kufanya lolote na pesa zangu. Au nyinyi mna wivu kwa sababu mimi ni mkarimu.”

**40.7** Hili ni fumbo.Mwenye shamba anafananiswa na Mungu. Mungu anawaita watu na atawalipa na uzima wa milele, wawe wamemhudumia kwa mda mrefu au mda mfupi. Hatutakiwi kulalamika kwa sababu ya mda wenye tumemhudumia Mungu eti tutalipwa zaidi.Kwa hivyo, nini itashinda malipo ya uzima wa milele.